LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# UWEZO WA KUSHITAKI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




**Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia**

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# UWEZO WA KUSHITAKI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


**SHUKRANI** .......... **5**

**DIBAJI** .......... **8**

**1. UTANGULIZI** .......... **10**

**2. MAANA HAKI YA KUSHITAKI** .......... **10**

**3. SHERIA INAYOTUMIKA** .......... **12**

**4. UMUHIMU WA UWEZO WA KUSHTAKI** .......... **12**

**5. NANI ANAWEZA KUSHITAKI AU KUTETEA** .......... **13**

**6. NANI ANAWEZA KUSIMAMA BADALA YA MTOTO** .......... **14**

**7. MASHARTI YANAYOTAKIWA KWA MWOMBAJI AU MLALAMIKAJI** .......... **15**

7.1.Uwezo wa Mahakama Kuzuia Wasiokuwa na Uwezo Kushitaki .......... 17

**8. HITIMISHO** .......... **19**

# SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasharia wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

# DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma yakusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pam oja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria am bayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.
Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafahdhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# 1. UTANGULIZI

Sheria inampa haki ya kushitaki mahakama mtu yeyote aliyetenda kosa au ambaye anaona kuwa haki yake ya msingi katika umiliki au katika jambo lolote imevunjwa, na kwamba mbinu au njia nyingine za usuluhishi zimeshindikana. Chombo chenye mamlaka ya kumaliza mashauri au mgogoro ni mahakama au mabaraza yeyote yaliyo na uwezo wa kimahakama. Hivyo basi ni ruksa kwa mtu yeyote mwenye haki ya kushtaki yaani ana husika na ana uwezo kupeleka shauri au mgogoro wake mahakamani kufanya hivyo. Haki ya kushtaki hujumuisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na uwezo kiakili, maslahi, na kiwango cha kuathirika.

# 2. MAANA HAKI YA KUSHITAKI

Haki ya kushitaki au "locus standi" in uwezo wa kisheria alionao mtu, kampuni au chombo chochote chenye haki ya kisheria ambayo imevunjwa. Haki ya kupeleka shauri mahakamani, kudai haki au maslahi yaliyo hatarini kupotea, au yaliyovunjwa ndio njia pekee ya kuhakiki uhuru na usalama wa raia na mali zao.

Kama haki ya kushtaki ni ya chombo mbali na mtu binafsi, kinahitajika kuwa kimesajiliwa chini ya sheria husika na kwamba kiwe kinafanya kazi kwa mujibu wa taratibu zote zinazohitajika. Mfano kama ni kampuni ni sharti kampuni hiyo iwe imesajiliwa chini ya sheria ya makampuni na iwe na leseni ya kufanya biashara au kazi kulingana na katiba yake. Na kama ni asasi ziwe zinasajiliwa kwa mujibu wa sheria za asasi ambazo ni:-

a. Sheria ya Makampuni (Sura ya 212 Mapitio ya 2002);
b. Sheria ya Asasi (Sura ya 337 Mapitio ya 2002);
c. Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini (Sura ya 318 Mapitio ya 2002);
d. Sheria ya Asasi za Zisizo za Kiserikali ya mwaka 2002.

KUMBUKA:

Kwa sababu vyombo vingine mbalimbali havina uhai kama alivyo binadamu basi uhai wa kampuni au asasi huwa unatekelezwa na wakuu wa kampuni au asasi. Wakuu hawa wanaweza kuwa Wakurugenzi, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu, Meneja au Watendaji wengine wowote waliopewa mamlaka katika kampuni au katika asasi.

## 3. SHERIA INAYOTUMIKA

Uwezo wa kusimama na kulinda haki upo chini ya sheria ya Uingereza ijulikanayo kama "common law" ambayo ilikuja kwa njia mapokeo na kuidhinishwa kutumika kwetu tangu mwaka 1922 chini ya sheria ijulikanayo kama Judicature and Application of Laws Act, (Sura ya 358 Mapitio ya 2002). Sheria hii bado inatumika kwani mpaka leo hatuna sheria iliyotungwa na bunge letu tukufu kuzungumzia katika ujumla wake suala la uwezo wa kushtaki.

## 4. UMUHIMU WA UWEZO WA KUSHTAKI

Haki au uwezo wa kushitaki ni njia ya taaluma ya sheria ya kuweka bayana nani anaweza kushitaki. Kwa jinsi hii sheria inafanya yafuatayo:-

a. Huweka bayana nani ana maslahi kwenye shauri;

b. Huzuia watu/chombo kisichokuwa na maslahi kufaidika na kitu chochote kitakachopatikana kutokana na shauri hilo;

c. Huwalinda watu wasio na makosa kuingizwa/

kuhusishwa na shitaka lililo mbele ya sheria;

d. Huzuia watu/chombo/maslahi ya mbali/kufikirika kutumia mahakama kama sehemu ya kujipatia maslahi; kutishia au kupata kitu chochote isivyo halali;

e. Huzuia msongamano wa mashauri mahakamani.

## 5. NANI ANAWEZA KUSHITAKI AU KUTETEA

Wafuatao ni watu wenye uwezo wa kushtaki:-

a. Mtu yeyote mwenye maslahi

b. Kwenye mashauri yanayohusu haki za binadamu na hasa hasa yanayowagusa watu wengi (public interest and class action) basi dhahiri kuwa asasi za kijamii kama NGO's, CBOs au mtu mmojawapo anaweza kuwa ana uwezo wa kushitaki. Mfano wa mashauri haya ni kama yale yanayogusa;

   i. Haki za wafungwa;
   ii. Haki za watoto;
   iii. Haki za Wakimbizi;
   iv. Haki za Wafanyakazi;
   v. Haki za wakulima, na wanajamii wa hali hiyo;

vi. Haki za watu wenye ulemavu;

vii. Haki za makundi mengine yaliyotengwa na jamii kutokana na hali yao waliyonayo. Mfano rangi, elimu, jamii, waathirika n.k.

ANGALIZO

Sheria inatambua kuwa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 huchukuliwa kuwa ni mtoto kwa hiyo basi ni dhahiri kisheria kuwa watoto hawana uwezo wa kusimama mbele ya sheria kushitaki au kutetea maslahi yao kwa sababu wanachukuliwa kutokuwa na uelewa wa kisheria.

## 6. NANI ANAWEZA KUSIMAMA BADALA YA MTOTO

a. Kutokana na taratibu za kisheria mtu yeyote wa karibu anao uwezo wa kusimama mbele ya mahakama kwa niaba ya mtoto ambaye ana maslahi katika shauri lililo mbele ya sheria. Mtu huyo huitwa rafiki wa mlalamikaji (next friend);

b. Vilevile wazazi/walezi wa mtoto wana uwezo wa kusimama mbele ya mahakama kushitaki au

kutetea shauri kwa maslahi ya motto;

c. Msimamizi wa mirathi pia anaweza kusimama na kushitaki au kutetea kwa niaba ya watoto.

## 7. MASHARTI YANAYOTAKIWA KWA MWOMBAJI AU MLALAMIKAJI

Ili mwombaji au mlalamikaji aweze kufaulu kushitaki au kutetea maslahi yake mahakamani bila ya pingamizi lolote la kutokuwa na uwezo ni sharti basi mwombaji au mlalamikaji atimize yafuatayo:-

a. Maslahi anayoyatetea mlalamikaji au mlalamikiwa yawe yanalindwa kisheria;
b. Maslahi ya mwombaji au mlalamikaji yaonekane kuingiliwa na mlalamikiwa;
c. Maslahi ya mwombaji au mlalamikaji yanayolindwa kisheria yaonekane kupotea au kunyang'anywa na mlalamikiwa;
d. Maslahi ya mwombaji au mlalamikiwa yanayolindwa kisheria yaonekane kutishiwa na kwamba tishio hilo litaathiri maslahi yake endapo litaachwa liendelee au litatimizwa na mlalamikiwa;

e. Mlalamikaji au mwombaji awe ameathirika kisheria au yuko hatarini kuathirika kisheria;

f. Mlalamikaji au mwombaji awe anawakilisha chombo maalum kama vile mwanasheria mkuu au polisi.

Angalizo

Ikumbukwe kuwa pale maslahi ya umma yanapoonekana kuvunjwa au yamo hatarini kuvunjwa basi mwanasheria mkuu au polisi kwa niaba ya jamhuri anao wajibu kwa uwezo wake mwenyewe kisheria kuyalinda maslahi ya umma. Kwa maana hiyo basi, pale sheria za nchi zinapovunjwa, mwanasheria mkuu au polisi ana wajibu wa kupeleka mashauri mahakamani kwa niaba ya Jamhuri. Na ndio maana mashtaka yote ya jinai yanawakilishwa na mwanasheria mkuu au polisi. Mwanasheria mkuu anao uwezo wa kukasimu mamlaka aliyopewa na sheria kwenye chombo kingine chochote chenye uwezo woa kufanya kazi hii. Mfano mzuri ni chombo cha polisi ambacho kimepewa uwezo huu na mwanasheria mkuu katika mashtaka ya jinai kadhaa.

Pale ambapo mwanasheria mkuu anaona hakuna maslahi ya umma yaliyovunjwa lakini mtu binafsi au kikundi cha watu kinaona kuwa kuna maslahi, basi mtu binafsi anaruhusiwa na sheria kupeleka maombi yake mahakamani ili aweze kuliendesha shauri hilo, mwanasheria mkuu anao uwezo wa kisheria kuliingilia shauri hilo na kuendelea nalo kwa niaba ya Jamhuri.

### 7.1. Uwezo wa Mahakama Kuzuia Wasiokuwa na Uwezo Kushitaki

Mahakama inao uwezo wa kuzuia au kumzuia mtu yeyote au chombo chochote kilicholeta shauri mahakamani baada ya kuridhika kwamba:-

a. Maslahi ya mwombaji ni ya kijumla mno kiasi kwamba kuathirika kwake au maslahi yake hayaonekani kupotea au kuathirika;

b. Maslahi ya mwombaji au mlalamikaji ni ya kufikirika "hypothetical";

c. Maslahi ya mwombaji au mlalamikaji ni ya kujaribu nadharia za kielimu. Hii ni kwa sababu mahakama ni chombo cha haki katika haki ambazo tayari ziko na zimezoeleka katika jamii; na wala si chombo cha kujaribisha haki ambazo hazipo na

haijaingia katika jamii;

d. Maslahi ya mwombaji au mlalamikaji yalishakufa;

e. Maslahi ya mwombaji au mlalamikaji ni maslahi kivuli “shadow interest”;

f. Maslahi ya mwombaji yanagusa kundi kubwa lakini katika maombi mwombaji au mlalamikaji analalamika kwa kujinufaisha peke yake.

Angalizo

Katika hali inayofanana na maelezo ya (f) hapo juu ni muhimu basi kuomba ruhusa ya mahakama kwa kufanya maombi maalumu na kama utaratibu uliowekwa kisheria hautufuatwa, basi maombi hayo yanaweza kutupiliwa mbali. Maombi ya kushtakiwa kwa niaba ya kikundi yanaweza kufanywa na mwombaji mwenye maslahi katika shauri akiungwa mkono na baadhi ya wanakikundi.

# 8. HITIMISHO

Kabla ya mtu au chombo chochote chenye uwezo wa kushitaki kama ilivyoelezwa hapo juu ni muhimu kabisa kujiridhisha kisheria kuwa katika shauri ambalo laelekea kupelekwa mahakamani lina sababu za kimsingi kabisa na limetimiza vionjo vya masharti yote yaliyotajwa hapo juu. Hii ni kuepuka hapo mbeleni uwezekano wa kulipa gharama pengine kuendeleza chuki zisizo za msingi.

Pia ni muhimu kukumbuka kuwa kama mtoto ana shauri na mtu mwingine na ana nia ya kupeleka shauri hilo mahakamani kwa niaba ya mtoto, ikumbukwe kwamba hawezi kupeleka shauri hilo moja kwa moja bila kupata ruhusa ya mahakama baada ya kuomba kufanya hivyo.

Ni matumaini yetu kuwa baada ya wewe msomaji kupata kijarida hiki na elimu juu ya uwezo wa kushitaki utaitoa kwa wengine.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV


*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*